

Ukweli Kuhusu Ukeketaji/Ukataji wa Wanawake (FGM/C)

Marekani imejitolea kumaliza Ukeketaji/Ukataji wa Wanawake (FGM/C). Ikiwa unaamini uko katika hatari ya Ukeketaji/Ukataji wa Wanawake FGM/C, unajua mtu aliye katika hatari ya Ukeketaji/Ukataji wa Wanawake FGM/C, una maswali kuhusu Ukeketaji/Ukataji wa Wanawake FGM/C, au umefanyiwa Ukeketaji/Ukataji wa Wanawake FGM/C na unahitaji msaada au maelezo zaidi, tafadhali wasiliana kwa nambari iliyo hapa chini.

Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) Ni Nini?

Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) inamaanisha kukata na taratibu zote zinazojeruhi viungo vya uzazi vya wanawake kwa sababu zisizo za kimatibabu. Pande zingine za dunia inaitwa “tohara ya wanawake”. Kitendo hicho hakina manufaa ya kiafya na kinaweza kusababisha matatizo ya afya ya kimwili au kiakili.

Madhara Ya Kiafya Ya Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) Ni Gani?

Madhara ya mwanzo yanajumuisha uvujaji damu, maumivu makali, na wakati mwingine kifo. Matatizo ya kiafya ya muda mrefu yanaweza kujumuisha maambukizo ya mkojo, nasuri, utasa, hedhi au maumivu wakati wa kufanya mapenzi, na kuongezeka kwa uwezekano wa kuambukizwa UKIMWI. Zaidi ya hayo, wanawake ambao wamepitia Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) wana uwezekano mkubwa wa kuwa na ugumu wakati wa kuzaa na watoto wao wana uwezekano mkubwa wa kufa kwa sababu ya kitendo hicho. Hatimaye, kitendo hicho mara nyingi huwaacha wasicha na wanawake wakiwa na woga, majeraha ya kisaikolojia, aibu, na huzuni.

Maoni ya Serikali ya Marekani Kuhusu Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) Ni Gani?

Serikali ya Marekani inapinga Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C), haijalishi aina, kiwango, au ukubwa wa kitendo hicho, na bila kujali lengo la kutekeleza kitendo hicho. Serikali ya Marekani inaelewa kwamba Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) unaweza kufanywa kulingana na tamaduni na kama sehemu ya unyago. Hata hivyo, Serikali ya Marekani inazingatia Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) kuwa ukiukaji wa haki za binadamu, na aina ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto.

Kwa Nini Marekani Inatoa Notisi Hii ya Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C)?

Marekani imejitolea kumaliza Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) ili kulinda afya na uzima wa, na kuendeleza haki za, wanawake na wasichana duniani. Marekani inajishughulisha nyumbani na katika nchi zingine ili kusaidia kuelimisha watu kuhusu madhara mabaya na hatari ya Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) kwa wanawake na wasichana.

Matokeo ya Jinai au Kusaidia Katika Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) Ni Gani?

Kuwafanyia wasichana chini ya umri wa miaka 18 Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C), au kuwatuma au kujaribu kuwatuma nje ya Marekani ili wafanyiwe Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) ni kinyume na sheria. Ukiukaji wa hii sheria kunaadhibiwa na hadi miaka 5 jela, faini, au zote mbili. Hakuna msamaha kwa kufanya Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) kwa sababu ya utamaduni. Ukataji na taratibu zingine zinazojeruhi viungo vya uzazi vya msichana aliye chini ya umri wa miaka 18 umepigwa marufuku na sheria za Marekani.

Matokeo ya Uhamaji Yanayotokana na Ukiukaji wa Sheria Dhidi ya Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) Ni Gani?

Ukiukaji wa sheria dhidi ya Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) – hata bila kushtakiwa kwa kosa la jinai – kunaweza kuwa na matokeo mabaya ya uhamaji, ikiwa ni pamoja na kumzuia mtu asiingie au kumtoa mtu kutoka Marekani, pamoja na kutostahiki kwa baadhi ya manufaa ya uhamaji.

Je, Wanawake Waliofanyiwa Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) Wamevunja Sheria Yoyote?

Msichana au mwanamke aliyefanyiwa Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) hana makosa yoyote. Hajakiuka sheria zozote za Marekani kwa kufanyiwa kitendo hicho. Ustahiki wa kusafiria au manufaa ya uhamaji kutoka Marekani hayaathiriwi ikiwa mtu amefanyiwa Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C).

Mtu Anaweza Kupata Nyenzo Zaidi Wapi?

Ikiwa unaamini kwamba uko katika hatari ya kufanyiwa Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) au umefanyiwa Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C), una maswali kuhusu Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C), una habari kuhusu mtu aliyefanyiwa Ukeketaji/Ukataji Wa Wanawake (FGM/C) nchini Marekani, au unajua mtu ambaye huenda akawa katika hatari ya kufanyiwa kitendo hicho hapa au nje ya Marekani, tafadhali wasiliana kwa nambari hii kwa maelezo zaidi kuhusu nyenzo zinazopatikana: **1-800-994-9662**